

SIKU ZA MATESO

Victor Murishiwa

Moderato

Shairi:

1. (a) Si ku za ma te so za ma te so ya ngu
(b) Ni li po li i ta ji na la ko Bwa na Mu ngu wa ngu,

Kiitikio:

na li ku li li - - a
u li i si ki - - a Mu ngu wa ngu, Ni ku shu ku ru je

Bwa - na, Ni ta m ke ne - - no ga ni mi mi?

2(a) Nikifikiria uliyonitenda (Mungu wangu) chozi la upendo lanitoka
(b) Umeniokoa kwenye maumivu (Mungu wangu) Ninarukaru-ka kwa furaha
Nikushukuruje.....

3(a) Uliyazibua masikio yangu (Mungu wangu) nikapata kusikia tena;
(b) Nayo macho yangu uliyafumbua (Mungu wangu) nikapata kutazama tena
Nikushukuruje.....

4(a) Marafiki zangu waliponiacha (Mungu wangu) Ulibaki name Mungu wangu;
(b) Nilipoanguka ulinipa nguvu (Mungu wangu) nikawa Imara mwenye nguvu.
Nikushukuruje....